# MFUKO WA JUMUIYA YA WATANZANIA

# COLUMBUS, OH

__________

# KANUNI ZA MFUKO

# KANUNI ZA MFUKO

# 2022

**1) UTANGULIZI ……………………………..……………………….……… 3**

**2) KUJIUNGA NA MFUKO …………………………………………..……..4**

**3) WAJIBU WA MWANAMFUKO ………………………………….……. 5**

**4) FAIDA ZA KUJIUNGA NA MFUKO …………………………..….. 9**

**5) KUACHA /KUFUTWA KUWA MWANAMFUKO……............... 11**

**6) HITIMISHO …..…………………………………………………..…….... 12**

**7) MAWASILIANO ……………………………………………………..…13**

**8) VIELELEZO ……………………………………………………………...14**

## 1. UTANGULIZI:

Mfuko wa Jumuiya ya Watanzania Ohio umesajiliwa na Serikali ya Jimbo la Ohio, kama "Tanzanian Columbus Community Association" kupitia katibu wa jimbo la Ohio tarehe 11, November 2011 kama taasisi isiyo ya kibiashara. Kwa kumbukumbu, nambari ya taasisi ni 2054369, na namba ya usajili wa mfuko ni 201129101154.

Mfuko utajiendesha na kuongeza mapato kwa kutegemea ada na michango kutoka kwa wanamfuko, miradi halali inayoshirikisha wanamfuko na wasio wanamfuko, na pia misaada ya kutoka watu binafsi, kampuni na taasisi zitakazopenda kuchangia maendeleo ya mfuko. Mfuko unaweka amana katika benki ya Chase, akaunti namba 2998302240 tawi la Easton Town Center; 4000 Morse Crossing, Columbus OH, 43219.

Madhumuni ya mfuko ni kumsaidia mwanamfuko bila ya kujali dini, itikadi ya kisiasa, kabila, ama jinsia ya mwanamfuko, pale anapopata matatizo ya;

i) Msiba wa ndugu wa mwanamfuko walio orodheshwa na mfuko

ii) Magonjwa sugu ambapo mwanamfuko ameugua kwa muda usiopungua miezi mitatu na kuwa katika hali ya kutoweza kujihudumia mwenyewe kwa mahitaji ya msingi katika maisha. Mgonjwa atahitajika kutoa ripoti na kidhibitisho kutoka kwa daktari.Uongozi utafanyia kazi ripoti hiyo ikiwa pamoja na kuhakiki. Baada ya kuridhika uongozi utatoa mafao.Endapo utatokea walakani wa ripoti hiyo uongozi una mamlaka ya kumyima mgonjwa mafao.

iii) Kesi za uhamiaji pale tu inapoamuliwa na mamlaka husika kwa mwanamfuko kuondolewa nje ya nchi na hivyo kuhitaji msaada wa kisheria. Mfuko utasaidia kuchangia sehemu ya gharama za mwanasheria baada ya mwanamfuko kuweka wazi nia yake ya kutaka utetezi wa mwanasheria katika mahakama ya Uhamiaji.

Mfuko utamsaidia mwanamfuko pekee na siyo ndugu ya mwanamfuko kwa matatizo yaliyoainishwa hapo juu. Pale mwanamfuko anapofariki, mfuko utamhudumia mrithi wa mwanamfuko aliye tambulishwa kwenye kumbukumbu za mfuko.

2. KUJIUNGA NA MFUKO:

a) Kujiunga na mfuko ni kwa hiari katika kipindi maalum cha kujiunga na mfuko. Sifa ama vigezo vya mwombaji kukubaliwa kuwa mwanamfuko ni kama ifuatavyo;

   i) Mwombaji awe ni raia wa Tanzania kwa namna zifuatazo; kwa kuzaliwa Tanzania; kuolewa ama kuoa mtanzania; raia wa Tanzania kwa kuandikishwa kupitia taratibu za uhamiaji; mtoto wa mtanzania kwa kutokana na njia za uraia wa Tanzania kama zilivyo ainishwa katika kipengele hiki

   ii) Mwombaji awe na umri wa kuanzia miaka 18 wakati wa kujiunga na mfuko

   iii) Mwombaji awe ni mkazi wa jimbo la Ohio

b) Mwombaji anapaswa kujaza kwa ukamilifu fomu maalumu ya kujiunga na mfuko inayopatikana kutoka uongozi wa mfuko. Kutakuwa na vipindi viwili vya kujiunga na mfuko (Jan 1st-31st) na (July 1st-31st)

c) Baada ya kujiunga na mfuko, sababu pekee zitakazo kubalika kubadili taarifa zilizo kwenye fomu ni; mwanamfuko kuolewa/kuoa, mwanamfuko kutoa/kupata talaka, mwanamfuko kupata mtoto/watoto, mabadiliko ya simu/anuani ya mwanamfuko, mabadiliko ya jina kisheria, na mwanamfuko anapofariki/ndugu wa mwanamfuko anapofariki.

d) Baada ya kukabidhi fomu kwa uongozi, mwanamfuko hatarusiwa kuongeza majina ya baba/mama/kaka/dada zaidi ya majina yaliyokwisha wakilishwa kwenye fomu wakati wa kujiunga na mfuko.

e) Ni wajibu wa mwombaji kuhakikisha anapata nakala ya kanuni za mfuko, kanuni za uongozi, na fomu ya kujiunga na mfuko toka uongozi wa mfuko. Mwombaji atawajibika kuwasilisha kwa uongozi fomu yake ya kujiunga na mfuko wakati wa kujiunga na mfuko.

f) Mwombaji ataweza kuwa mwanamfuko baada ya kuwa na sifa zilizotajwa hapo juu na kukamilisha kulipa ada ya kujiunga na mfuko. Ada ya kujiunga na mfuko ni jumla ya $50 kwa yeyote anayejiunga, pasipo kutegemea mwombaji amejiunga mwezi upi ndani ya mwaka.

g) Majumuisho ya $50 ya ada ya kujiunga na mfuko yanatokana na ada ya kuandikishwa ya $10 inayotolewa mara moja tu wakati wa kujiunga na mfuko kwa mara ya kwanza, na salio la $40 ni ada ya mwaka itakayotolewa kila mwaka kwa kipindi chote mhusika ataendelea kuwa mwanamfuko. Mkutano mkuu wa wanamfuko wote ndiyo kikao pekee chenye maamuzi ya kubadili kiwango cha ada ya mwaka ya $40 kwa kila mwanamfuko.

h) Ili kuendelea kutambulika kuwa mwanamfuko, mhusika atapaswa kuzingatia na kufuata kanuni za mfuko ikiwa ni pamoja na kulipa ada za mwaka na michango ya harambee kadiri inapotokea kufuatana na kanuni za mfuko na kuhudhuria vikao vya wanamfuko wote vinavyofanyika katika mwaka.

3. WAJIBU WA MWANAMFUKO:

a) Katika kufanikisha na kuharakisha huduma kwa mwanamfuko, ni wajibu wa mwanamfuko kuufahamisha uongozi kwanza, pale anapopata matatizo yafuatayo;

   1) Msiba wa ndugu wa mwanamfuko walioorodheshwa na mfuko

   2) Magonjwa sugu ambapo mwanamfuko ameugua kwa muda usiopungua miezi mitatu na kuwa katika hali ya kutoweza kujihudumia mwenyewe kwa mahitaji ya msingi katika maisha.Mgonjwa atahitajika kutoa ripoti na kidhibitisho kutoka kwa daktari.Uongozi utafanyia kazi ripoti hiyo ikiwa pamoja na kuhakiki.Baada ya kuridhika uongozi utatoa mafao.Endapo utatokea walakani wa ripoti hiyo uongozi una mamlaka ya kumyima mgonjwa mafao.

   3) Kesi za uhamiaji pale tu inapoamuliwa na mamlaka husika kwa mwanamfuko kuondolewa nje ya nchi na hivyo kuhitaji msaada wa kisheria. Mfuko utasaidia kuchangia sehemu ya gharama za mwanasheria baada ya mwanamfuko kuweka wazi nia yake ya kutaka utetezi wa mwanasheria katika mahakama ya Uhamiaji.

b) Mwanamfuko ana wajibu wa kuhakikisha uongozi unapata taarifa za mabadiliko ya kumbukumbu zake mwanamfuko kwa wakati muafaka, pale inapotokea mtoto/watoto wa mwanamfuko kuzaliwa, mwanamfuko kuoa/kuolewa, mwanamfuko kuwa na talaka ya mume/mke, mabadiliko ya jina kisheria, na pia yanapotokea mabadiliko ya simu ama anuani ya mwanamfuko.

c) Mwanamfuko ana wajibu wa kufuata kanuni zote za mfuko, na kushiriki shughuli zote zinazoandaliwa na mfuko, ikiwa ni pamoja na kuhudhuria mikutano, sherehe za kuongeza mapato ya mfuko, kuhani misiba, na kufarijiana katika matatizo mbalimbali yanapotokea miongoni mwa wanamfuko wenzetu.

d) Mwanamfuko ana wajibu wa kulipa ada na kushiriki kutoa michango ya harambee kwa wakati muafaka ili kufanikisha majukumu ya mfuko katika kusaidia mwanamfuko aliyepata tatizo la kuhitaji kuhudumiwa na mfuko kufuatana na kanuni za mfuko.

e) Baada ya kujiunga na mfuko, kwa kila mwaka unaofuata, mwanamfuko atatakiwa kulipa ada ya mwaka na kutimiza masharti yote ya kipengele 2 ibara (h) ili kumfanya aendelee kutambulika kuwa mwanamfuko kwa utaratibu ufuatavyo;

i) Ada ya mwaka pasipo faini ni $40, na inatakiwa kulipwa ndani ya kipindi cha mpito, kuanzia Januari 1 – Januari 31 ya kila mwaka.Hii nawajumuisha pamoja na wanamfuko waliojiunga July ya mwaka uliotangulia. Kwa mwanamfuko anayejiunga kwa mara kwanza, ada ya mwaka kwa mwezi wowote atakaojiunga na mfuko ni $50. Mwaka unatambulika kuanza Januari – Desemba.

ii) Malipo yoyote ya ada ya mwaka yatakayofanyika ndani ya mwezi Februari, yataambatana na faini ya $20 na kuifanya jumla ya ada ya mwaka kuwa $60 kwa mwanamfuko atakayelipa ada ya mwaka ndani ya mwezi Februari.

iii) Kama mwanamfuko atalipa ada yake ndani ya mwezi Machi, atatakiwa kulipa ada ya $40 pamoja na faini $40, na kuifanya jumla ya ada ya mwaka kuwa $80 kwa mwanamfuko atakayelipa ada ya mwaka ndani ya mwezi Machi.

iv) Hivyo, mwanamfuko ana nafasi ya kulipa ada ndani ya miezi mitatu kuanzia Januari 1 - Machi 31. Baada ya hapo, mfuko hautaweza kumsaidia kwani kwa kutolipa ada yake ya mwaka katika miezi mitatu ya mwanzo, kutamfanya mwanamfuko kuwa amejiifuta rasmi na mfuko kuanzia April 1.

v) Katika kipindi cha miezi mitatu ya mwanzo ya ulipaji ada ya mwaka, mfuko utamhudumia kikamilifu mwanamfuko yeyote aliyepatwa na tatizo la kuhitaji

msaada wa fedha kufuatana na kanuni, iwapo tatizo hilo litatokea kati ya januari 1 – januari 31.

vi) Kwa kuwa malipo ya ada ya mwaka yatakayofanyika kuanzia Februari 1 – March 31 yataambatana na faini, basi mwanamfuko atakatwa kiasi cha hela anachodaiwa na faini yake kutoka kwenye $2000 kwa mwanamfuko atakayekuwa hajalipa ada yake ya mwaka na amepata tatizo la kuhitaji msaada wa fedha kufuatana na kanuni za mfuko. Pia, mfuko utatumia hiyo nusu ya mafao kulipa malimbikizo ya madeni yoyote ya mhusika, ikiwa pamoja na kulipia ada yake ya mwaka kabla ya kukabidhiwa salio lake la fedha.

vii) Baada ya kujifuta na mfuko kwa misingi ya kutolipa ada, au kwa hiari (Rejea Kifungu namba 5:2) mwanamfuko anaweza kujiunga tena na mfuko kwa kulipa $150 (faini $100, kiingilio $10 na ada $40) ikiambatana na madeni yote aliyoacha alipokuwa mwana mfuko. Muda ambao anaruhusiwa kurudi ni Jan 1- January 31 au July 1 –July 31.

f) Kila mwanamfuko anawajibu wa kuwasilisha mchango wake wa $20 ndani ya siku 30 (mwezi mmoja) tokea siku taarifa ya msiba/kesi ya uhamiaji/ugonjwa kutangazwa na uongozi wa mfuko. Mwanamfuko anayefanyiwa Harambee pamoja na mke/mume/mtoto/mzazi hawata takiwa kutoa mchango wa $20 (Rejea kifungu cha 4;(e)). Harambee zote zitakazotangazwa na uongozi na ni wajibu wa kila mwanamfuko kushiriki.

g) Kama mwanamfuko hajakabidhi mchango wake ndani ya siku 30 (mwezi mmoja) kutokea siku taarifa ya tatizo kutangazwa na uongozi wa mfuko, mwanamfuko atatakiwa kutoa mchango wake wa $20 pamoja na faini ya $10 kwa kila mwezi wa kalenda utakaofuata kwa muda atakaochelewa kutoa mchango wake. Endapo kutatokea zaidi ya tatizo moja (eg; msiba) ndani ya mwezi mwanamfuko atatakiwa kulipa faini ya tatizo la kwanza tu. Kiwango cha juu cha faini kinachokubalika kwa mwanamfuko ni jumla ya $50 (miezi 5 ya kalenda kutoka siku uongozi ulipotangaza taarifa ya tatizo), vinginevyo mwanamfuko atakuwa amejifuta mfuko kwa hiari yake mwenyewe. Uongozi una wajibu wa kukumbushia michango kwa wanamfuko kila mara, na pia ni jukumu la uongozi kuongeza muda wa michango iwapo matatizo yataongozana.

h) Malipo yoyote kwa mfuko yanaweza kufanyika kwa njia ya kuweka amana katika benki ya chase, akaunti # 2998302240, ama kupitia malipo ya paypal kwa anuani

ya jumuiyatanzaniaohio@yahoo.com, https://jumuiyatanzaniaohio.org ama kupitia quickpay kwa anuani ya jumuiyatanzaniaohio@yahoo.com, kupitia tovuti ya tcca ama kukabidhi fedha kwa mjumbe yoyote wa kamati ya uongozi wa mfuko. Ruksa kwa mwanamfuko kutoa in advance kuanzia $100 na zaidi kwa ajili ya kuepukana na michango ya kila mara. Mwanamfuko atapaswa kuujulisha uongozi wa mfuko mara tu baada ya kutuma fedha. Kama mwanamfuko ana matatizo ya kutoa michango yake kwa wakati anapaswa kuujulisha uongozi mapema.

i) Pale mwanamfuko atakapoamua kufanya malipo kwa kutumia hundi, ni wajibu wa mwanamfuko kuandika hundi kutoka akaunti yenye fedha za kukamilisha malipo kwa hundi anyoandika. Kama hundi haitapita kwa upungufu wa fedha, mwanamfuko atawajibika kufanya tena malipo, yakiambatana na faini ya $30.

j) Kama mwanamfuko atakabidhi hundi isiyo na fedha kwa matukio mawili, mfuko hautakubali tena malipo ya hundi kutoka kwa mwanamfuko huyo. Mwanamfuko huyo, atalazimika kufanya malipo kwa njia ya fedha taslimu, malipo ya kupitia kadi, na malipo kupitia hawala ya fedha.

k) Kila mwanamfuko ana wajibu wa kuhudhuria mikutano yote, uchaguzi wa viongozi, harambee zote, na shughuli zote zinazoandaliwa na mfuko zinazohitaji ushiriki wa wanamfuko. Kila mwanamfuko anapaswa kuzingangatia muda kwa faida ya wanamfuko wote. Tafadhali fika mapema katika shughuli zote za mfuko, ili shughuli zikamilike kwa wakati kufuatana na ratiba ya shughuli husika.

l) Mwanamfuko atakayeshindwa kuudhuria mikutano yote miwili ya mwaka atatakiwa kulipa fee ya kujiunga tena ya $100 (badala ya $40) ili kuweza kuendelea kuwa mwanachama

m) Kila mwanamfuko ana haki na wajibu wa kupatiwa taarifa za fedha/maendeleo ya mfuko, kutoa maoni ya kuboresha mfuko, kupiga/kupigiwa kura kwenye chaguzi na mikutano mingine kwa mujibu wa kanuni za mfuko. Pia, kila mwanamfuko ana haki ya kugombea/kuchaguliwa katika nafasi yoyote ya uongozi wa mfuko kulingana na kanuni za mfuko.

n) Kila mwanamfuko ana wajibu wa kusoma kanuni za mfuko, kuzielewa, na kisha kusaidia kuutangaza mfuko na faida zake miongoni mwa watanzania wanaohamia Columbus na miji ya jirani, na pia watanzania walio na makazi Columbus na miji ya jirani lakini bado hawajajiunga na mfuko.

4. FAIDA ZA KUJIUNGA NA MFUKO:

a) Mfuko utamsaidia mwanamfuko na siyo ndugu wa mwanamfuko. Madhumuni ya mfuko ni kumsaidia mwanamfuko kwenye matatizo ya;

1) Msiba wa ndugu wa mwanamfuko walioorodheshwa na mfuko. Ndugu watakaokubalika kuorodheshwa na mfuko ni;

i) Baba mzazi/mlezi wa mwanamfuko

ii) Mama mzazi/mlezi wa mwanamfuko

iii) Mke/mume wa mwanamfuko

iv) Mtoto/watoto wa mwanamfuko

v) Dada/Kaka wa mwanamfuko

***Ufafanuzi wa mwanamfuko ni kama ifuatavyo: Mzazi mlezi ni mzazi aliyekulea wewe tokea utotoni, badala ya wazazi wako iwapo walifariki, mwanamfuko akiwa chini ya umri wa miaka 18. Mzazi mlezi ni mtu aliyechukua jukumu au aliyeteuliwa na mahakama kuwasilisha na kulinda maslahi ya mwanamfuko tokea utotoni (chini ya miaka 18) au wazazi walipofariki mwanamfuko akiwa chini ya unri wa miaka 18. Itakapohitajika mwanamfuko atatakiwa kutoa vithibitisho vya kuonyesha uhalali wa Mzazi mlezi kwa uongozi.

***Ufafanuzi wa Mtoto/Watoto/Mtegemezi/Wategemezi wa mwanamfuko ni kama ifuatavyo: Mtoto/Watoto wa kuzaliwa na mwanamfuko aliye/walio chini ya miaka 18. Au mtoto/Watoto chini ya miaka 18 anayepokea/wanayepokea msaada kutoka kwa mwanamfuko (kama vile mzazi), baada ya mahakama kumpa mwanamfuko dhamana. Au Mtoto/Watoto chini ya miaka 18 aliyeasiliwa/walieasiliwa na mwanamfuko. Itakapohitajika, mwanamfuko atatakiwa kutoa vithibitisho vya kuonyesha uhalali kwa uongozi.

2) Magonjwa sugu ambapo mwanamfuko ameugua kwa muda usiopungua miezi mitatu na kuwa katika hali ya kutoweza kujihudumia mwenyewe kwa mahitaji ya msingi katika maisha.Mgonjwa atahitajika kutoa ripoti na kidhibitisho kutoka kwa daktari.Uongozi utafanyia kazi ripoti hiyo ikiwa pamoja na kuhakiki. Baada ya kuridhika uongozi utatoa mafao.Endapo utatokea walakani wa ripoti hiyo uongozi una mamlaka ya kumyima mgonjwa mafao.

3) Kesi za uhamiaji pale tu inapoamuliwa na mamlaka husika kwa mwanamfuko kuondolewa nje ya nchi na hivyo kuhitaji msaada wa kisheria. Mfuko utasaidia kuchangia sehemu ya gharama za mwanasheria baada ya mwanamfuko kuweka wazi nia yake ya kutaka utetezi wa mwanasheria katika mahakama ya Uhamiaji.

b) Kama mwanamfuko amepatwa na tatizo lolote kati ya matatizo yaliyoainishwa hapo juu, mfuko utatoa $2000 kwa kila tukio ili kumsaidia mwanamfuko kukabiliana na gharama za awali. Kisha, uongozi wa mfuko utawashirikisha wanamfuko kwa njia ya harambee kuchangia/kufanikisha mahitaji ya fedha inayohitajika katika kuhudumia tatizo lililompata mwanamfuko husika. Mwanamfuko anawajibu wa kuufahamisha uongozi wa mfuko kiwango maalumu cha fedha kinachohitajika kutatua tatizo lake, ili uongozi uweze kuratibu mipango ya kufanikisha kuchangia kupitia wanamfuko.

c) Viongozi wa juu wa mfuko Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina watapata ongezeko la asilimia 25% na wajumbe wengine 5 wa kamati watapata ongezeko la asilimia 20% ya mafao anayopata mwanamfuko wa kawaida akipatwa na matatizo.

d) Rambirambi za nyumbani, ama fedha zitakazopatikana nyumbani kwa mwanamfuko aliyepatwa na tatizo hazitahusiana na mchango kutoka mfuko.

e) Kwa familia zenye wanamfuko zaidi ya mmoja katika mfuko, ndugu wote waliowanamfuko hawatachangia $20 za harambee pale tu inapotokea wamefiwa na ndugu anayewahusu wote, na ni ndugu aliyeorodheshwa kwenye kumbukumbu za mfuko na ndugu wote walio wanamfuko, ama mmojawapo wa ndugu hawa amepatwa na ugonjwa/magonjwa sugu ya kushindwa kuweza kujikimu kimaisha, ama amepatwa na kesi ya uhamiaji inayopelekea mhusika kuondoka nje ya nchi na hivyo kuhitaji msaada wa kisheria kufuatana na kanuni za mfuko.

f) Kwa familiya zenye wanamfuko zaidi ya mmoja katika mfuko, ndugu wote walio wanamfuko kila mmoja atapewa $2000 kutoka kwenye mfuko pale inapotokea wamepata msiba wa ndugu anayewahusu wote, na ni ndugu aliyeoorodheshwa na kila mwanafamiliya aliye kwenye mfuko. Kama kuna mahitaji ya ziada ya kifedha kwa familiya kutokana na msiba unaohusisha ndugu aliyeoorodheshwa na wanamfuko walio ndugu, mfuko utafanya harambee kwa kuzingatia uzito wa mahitaji ya ndugu wote walio katika mfuko kwa pamoja.

g) Kama wana-ndoa mmojawapo si mwanamfuko, mfuko utamsaidia yule tu aliye kwenye mfuko kwa matatizo yatakayo mpata yeye binafsi kama mwanamfuko, ama ndugu wa kuoorodheshwa na mwanamfuko huyo. Kama ndugu wa mke/mume asiye mwanamfuko atapata tatizo, mfuko hauna wajibu wa kutoa msaada wowote, na ni wajibu wa mume/mke aliye kwenye mfuko kumshawishi mwenziwe kujiunga na mfuko ili kuweza kuhudumiwa na mfuko kufuatana na kanuni za mfuko.

h) Mwanamfuko anapofariki, mfuko utatoa kiasi cha $15,000 kwa mrithi mmoja tu aliyeandikwa kwenye fomu ya kujiunga na mfuko.Kila mwanamfuko atachangia $100 ndani ya siku 60.Itakopotokea misiba imeongozana uongozi utatoa muda wa nyongeza kulipia $100.Pia Itakapotokea mrithi amefariki kabla ya mwanamfuko kufariki, mwanamfuko atatakiwa kuwasilisha kwa uongozi jina lingine la mrithi mmoja tu. Kama mrithi atafariki pamoja na mwanamfuko, uongozi utaamua ni ndugu yupi katika orodha ya ndugu wa mwanamfuko atakabidhiwa $15,000 kutoka katika mfuko. Mfuko hautatoa mafao yoyote kwa mrithi iwapo kifo cha mwanamfuko kimetokana na mwanamfuko kujiua.

i) Kwenye mkutano wa Januari 2017 wanamfuko walikubaliana kwamba inapotokea msiba katika jumuiya yetu ya Columbus kwa mtu asiye mwanachama hakutokuwa na mchango kutoka kwenye mfuko. Bali uongozi utajitolea kuhamasisha wanamfuko kuchangia msiba huo and vile vile kukusanya michango ya hiyari pale inapobidi.

j) Kwenye mkutano wa Januari 31,2020 wanamfuko walikubaliana kwa kauli moja kwa wanamfuko wapya watakaojiunga na mfuko kuanzia Julai 1st,2020 kutakuwa na siku 90 za kusubiri kabla hawajastahili kupata mafao ya aina yoyote. Iwapo itatokea mwanamfuko au wanamfuko wapya watapata msiba kabla hawajamaliza siku 90 mfuko hautatoa mafao ya aina yoyote.

5. KUACHA/KUACHISHWA KUWA MWANAMFUKO:

1. Mwanamfuko kwa mapenzi yake mwenyewe ana haki na hiari ya kuacha kuwa mwanamfuko wakati wowote atakavyoamua kufanya hivyo. Mwanamfuko anapoamua kuacha mfuko, hatarudishiwa ada ama michango yake aliyoitoa kwenye mfuko.

2. Mwanamfuko atakuwa amejifuta na mfuko pale atakapokuwa hajalipa ada yake ya mwaka baada ya kupita miezi mitatu ya mwanzo katika mwaka. Kufuatana na kanuni za mfuko, kuanzia April 1 ya mwaka, mwanamfuko asiyelipa ada ya mwaka atakuwa ameachana na mfuko. Mwanamfuko atakuwa amejifuta kutoka mfuko

kwa hiari yake mwenyewe iwapo atalimbikiza jumla ya faini ya $50 kutokana na michango ya harambee. Mwanamfuko anapojifuta na mfuko, hatarudishiwa ada ama michango yake aliyoitoa kwa mfuko.

3. Pale utakapogundulika ubadhilifu wa fedha ama udanganyifu wa taarifa za mwanamfuko ili kujipatia manufaa binafsi, uongozi una mamlaka ya kuchuckua hatua za kisheria kwa mhusika, ikiwa ni pamoja na kumuondoa kutoka katika mfuko.

4. Ni mkutano mkuu wa wanamfuko wote pekee wenye madaraka ya kuamua kufutwa kwa mfuko. Mkutano wa kuamua kufutwa kwa mfuko unapaswa kuhudhuriwa na zaidi ya nusu ya wanamfuko wote, na kupigiwa kura zaidi ya nusu ya wanamfuko waliohudhuria Mkutano.

5. Kwa mwanachama anayehama nje ya state ya Ohio ataendelea kuwa mwanachama na kupata faida za uanachama mpaka mwisho wa mwaka aliohama (mfano mwanachama akihama Januari 2017 ataendelea kuwa mwanachama mpaka Desemba 2017.

6. HITIMISHO:

Mwanamfuko yoyote ana haki ya kupendekeza Mabadiliko ya kanuni. Maamuzi ya kufanya mabadiliko ya kanuni yatapitishwa na mkutano mkuu wa wanamfuko wote pale tu mahudhurio ya wanamfuko hai yatakuwa ni zaidi ya nusu ya wanamfuko wote, na kupigiwa kura na zaidi ya nusu ya wanamfuko waliohudhuria mkutano. Mfuko unazingatia na kuheshimu faragha na usiri wa taarifa juu ya masuala nyeti, hasa kuhusiana na habari/taarifa binafsi zinazohusu wanamfuko.

## MAWASILIANO:

jumuiyatanzaniaohio@yahoo.com

https://jumuiyatanzaniaohio.org

Address:

TCCA

PO BOX 936

Worthington OH 43085

Chase Bank Account # 2998302240

Kamati ya Uongozi – 2018/2020

Lusajo Kibonde

**MWENYEKITI**

McDonald Mutta Lubago

**KATIBU**

Allan Anthony Rwabutaza (Dr.)

**MWEKA HAZINA**

David Mbaga

**MJUMBE**

Edgar Mjengwa

**MJUMBE**

Pamela Mwailolo

**MJUMBE**

Rose Odemba

**MJUMBE**

Vera Teri

**MJUMBE**